HABARI ZA POPOTE

Peru : Sherehe za Noeli kapigwa marufuku

Wahuni waliwashitumu wakaaji wa kijiji cha Oroya nchini Peru wasisherekee siku kuu ya Noeli. Wakaaji hao hawakusherehekea siku kuu hiyo sababu ya kuogopa kupoteza maisha yao. Kusudi la wahuni ni la kulazimisha watu kutupilia mbali desturi za kikristu na kutegemea zile zilizo bora za asili.

Pia watu wa Shirikisho la Amerika walitumia dolari miliari 39 kununua vifaa kazaa vya kusherehekea siku kuu ya Noeli. Kwa wastani (en moyenne) matumizi ya kila jamaa kwa jambo hilo yalikuwa dolari 335.

Uyahudi : Misaada ya Amerika yapingwa

Waziri wa uchumi Itzhak Modaï kanena kwamba Serkali ya Uyahudi yaweza kukataa misaada ya Shirikisho la Amerika ikiwa linaendelea kusaidia pia Wapalestina ambao wasisitiza juu ya kuundwa kwa taifa lao nchini Uyahudi. Yajulishwa kuwa Shirikisho la Amerika husaidia kifeza na kivyombo kwa namna ya pekee serkali ya Uyahudi.

Ethiopia : Watu milioni moja hatarini !

Kutokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe na ukame, zaidi ya watu milioni moja wapo katika hatari ya kufa na njaa nchini Ethiopia. Vita hivyo huendeshwa tangu miaka kazaa na wahuni wa sehemu za «Tigré na Erythrée» wakigombea uhuru wao toka hapo kuunda taifa lao.

Pia, nchini Sudania zaidi ya watu milioni tatu waangamizwa na njaa kutokana na vita viendeshwako pia. Na nchini Musumbiji zaidi ya watu 500.000 watezamiwa kufariki dunia na njaa kuwa vita mahali pengi vyapinga mlimo wa vyakula.

Panama : Huenda Noriega akahukumiwa kifungo cha miaka 140

Kutokana na kitendo haramu cha kupokonya haki za watu, kuendesha uchuuzi wa kimagendo wa madawa ya kulevya na kuteketeza maisha ya binadamu dikteta (dictateur) Jemadari Emanueli Noriega, raïs wa Panama hapo majuzi, alinaswa na waaskari wa Shirikisho la Amerika. Kwa sasa ndiyo azabu kwa matendo maovu kafanya kuwa atahukumiwa kifungo cha miaka 140 katika Shirikisho hilo. Raïs George Bush wa Shirikisho la Amerika katuma kweli waaskari-jeshi nchini huko na kumshika mateka dikteta huyo.

Walikale : Watu 15 wamepoteza maisha yao

Kutokana na msiba wa gari barabarani Walikale - Bukavu watu 15 wamepoteza maisha yao na wengine kazaa kaumia.

Pia, yajulishwa kuwa watu 21 walifariki dunia kutokana na misiba ya gari mjini Bukavu mwaka jana, watu 81 kajeruhiwa vikali na wengine 30 kapata vidonda vidogo vidogo.

Ulaya ya mashariki : Watu hudai demokrasia

Kulingana na kupinga kwa watu siasa ya kikoministi, siasa ya kidikteta, kwa kudai democrasia na uhuru, siku hizi kuna mabadiliko kazaa katika uongozi wa Serkali za nchi za Ulaya ya mashariki (*Ujerumani ya mashariki, Rumania, Chekoslovakia, Albania, Polonia* na Bulgaria). Kwa matendo haramu kafanya nchini raïs wa Rumania, Céaucescu hapo majuzi na mkewe katungikwa.

Pia barani Ulaya ya mashariki na penginepo ulimwenguni, maraïs na viongozi wadikteta (dictateurs) walirushwa madarakani na kujibu mashtaka yao. Na, ikiwa wengine walio bado madarakani hawabadili mfumo wa siasa za uongozi wao haratezamiwa kama siku si nyingi watatengwa na kulazwa.

Kivu ya Kusini : NJAA YAANGAMIZA WAKAAJI

Katika jimbo la Kivu ya Kusini yaani mitaani Kabare, Walungu, Fizi, Shabunda, Mwenga na mji wa Bukavu, maisha ya wakaaji huhatarishwa kwa kuwa waangamizwa na njaa, sawa vile mwaka wa 1984.

Baada ya kutoa ripoti kuhusu jambo hilo, Mwenyekiti wa Baraza la jimbo la Kivu ya Kusini, mwananchi Chimanuka Ntagayangabo alitoa hapo majuzi malalamiko yake kwa wataalam wa mlimo, viongozi wa kazi za Serkali jimboni na wa mashirika kusudi ya kusimika mipango ya kupambana namna ya pekee na njaa. Na hiyo kusudi ya kuokoa haraka umma ulio hatarini.

Moja ya ripoti hizo ambayo yaeleza mazao mabaya ao mavuno mabaya ya mlimo mwaka jana, hasa ya maharagwe, mihogo, mtama, viazi vya asili... katika kijiji cha Kajeje, mtaani Kabare ambako watu 37 walifariki dunia na njaa mwaka huo, watu 54 waligonjwa «bwaki» na jamaa 62 zilihama kijiji hicho kutokana na jambo hilo haramu.

Kuhusu mtaa wa Walungu, wakaaji wa mtaa huo huja mjini Bukavu kununua vyakula ambavyo bei yavyo hupanda siku kwa siku kama mruko wa kunguru.

Pia, kutokana na kuacha kulima na kuhusika kuchimba zahabu, wakaaji wa mitaa ya Mwenga na Shabunda pia huanza kuja mjini Bukavu kununua mihogo, mchele na maharagwe ingawa zamani vyakula hivyo katoka kwa wingi mitaani hiyo. Kwa mfano mfuko mmoja wa unga wa mihogo unanunuliwa kwa bei ya zaïres 25.000 mtaani Mwenga na kilauri kimoja cha mchele ni zaïre 100.

Kuhusu mtaa wa Fizi, yasemekana kwamba kuna uhaba na ukosefu wa mimea ya mihogo ambayo yameteketezwa na ugonjwa.

Kwa kifupi, njaa hiyo imetokana na mvua nyingi kazaa kanyesha, kipwa ao uhame wa jua kali, magonjwa ya mimea na kusafirishwa nchi za kigeni vyakula.

Toka, hali hiyo yawasukuma viongozi wa jimbo, wa nchi na wa dini kuchukua namna ya pekee mipango ya kweli.

Na Chirume Simba

Adabu za saa zote : DEREVA AO MTEMBEZA GARI

Hapa tutasimulia juu ya yule ambaye gari si lake, yule ambaye kutembeza gari ndio kazi yake. Maana yake yule anayetumikia mtu mwengine ao shirika fulani.

Ukiwa dereva jua kama gari lile si lako na kama bila lile utabaki «mlofwa». Ndio maana daraka zako ni za aina mbili.

Kwanza : kwa kuwa gari si lako upo mtumishi tu na sio mwenyeji. Kumbe azimio la utumizi wa gari halitatoka kwako wewe bali kwa mwenyeji. Kazi yako wewe ni kuongoza gari kulipeleka kule ambako waliliainisha, kwa mda wa kufaa na kwa kazi ikifwatana na kawaida ya mwenyeji.

Pili : kwa kuwa gari hilo ndio lako hauna kulitunza vema ili usikose kazi na matunda ya kazi yako yasikuepuke.

Ukiwa dereva wa «voiture» ao wa «auto-bus», na kazalika, onyesha kama umeadibika ukimpatia kila moja hekima yake. Watu unaowabeba garini mwako si watu wako, si watumishi wala watu chini ya uwezo. Sivyo. Wakiwa katika «auto-bus» ni sababu walilipa safari yao. Wale ambao unabeba katika «voiture» ni sababu mwenyeji alikuambia uwasafirishe. Wanaweza kuwa ndugu zake, marafiki ama wakubwa wake wa kazi ao wakubwa wa Serkali. Kumbe wakati ule ni wenyewe ndio wenyi kumiliki gari, ni wenyewe ndio wenyi kuhukumu, ndio wenyi uwezo juu ya gari. Uwe, mwenyi adabu kwao : usisimame mahali bila ruhusa yao, ufuate njia yao na usifuate yako binafsi. Katika maneno na matendo yako malezi mema na mwenendo bora vionekane, vikufanye mpendelevu mbele ya wageni wale.

Unaposafirisha akina-bibi hauna budi kuwa mvumilivu. Ujisahau mwenyewe binafsi kwani bila sadaka hiyo masikilizano ni mwiko. Pia ni daraka yako kulinda siri. Unaposafirisha wakubwa wako ao akina-bwana wengine, hebu ulinde siri. Usivumbue siri zao kwa kuwa ulizisikia linda ulimi wako usijipoteze matumaini.

Ukiwa dereva wa shirika fulani na kama unapashwa kusafirisha mwenzako wa somo ao wa kazi lakini mwenyi kukupita cho umheshimie ukif uata njia ambazo ao ambao anakupasulia yeye. Usijiruhusu kukamata wasafiri na kuwabeba garini bila ruhusa yake, usisimame pale upendapo bali akuambiapo usimame. Kwani kwa mda mnapokuwa pamoja ni yeye mnyampara wa shirika na wa wakubwa wa shirika.

Maneno yako yawe kamili na matendo yako bora. Usitamke maneno ya washerati unapobeba wakubwa wako wa kazi na unapopita penyi mji usiwapigie wasichana yowe. Kwani mwenendo wa aina hiyo ni ishara ya maadibisho mabaya na ni dalili ya kukosewa hekima.

Kimengele Kimode

BENKI KUU YA ZAIRE KAFUNGUA SOKO LA UNUNUZI WA ZAHABU

Ukomo wa Benki kuu la Zaïre kwa kununua zahabu ni kuipatia nchi ya Zaïre feza nyingi za kigeni, kanena Liwali wa Benki hilo mwanchi Pay-Pay wa Syakassighe ambaye hapo majuzi kafungua kiserkali soko la ununuzi wa zahabu mjini Bukavu. Soko ambalo laendeshwa chini ya uchunguzi wa tawi la Benki kuu la zaïre mjini Bukavu.

Kutokufaulu kwa siasa ya uhuru wa kuchimba, kununua na kuchuuza madini nchini baada ya miaka 5 ya majaribio na uchuuzi wa kimagendo wa zahabu hiyo katika masoko ya kigeni umesababisha ukosefu na uhaba wa zahabu hiyo hiyo nchini.

Chirume Simba